# Ukeketaji kwa Wanawake

## Female Genital Cutting

Swahili/Kiswahili

Parenting SA

**Ukeketaji kwa Wanawake (FGC) ni kinyume cha sheria katika majimbo yote nchini Australia. Pia ni kinyume cha sheria kumchukua msichana na kumpeleka nchi nyingine ili kukeketwa. Kitendo hiki huathili afya na maisha bora ya wasichana na wanawake.**

## Ukeketaji ni nini?

Ni kitendo cha kukata au kuondoa sehemu au viungo vyote vya nje kwenye uke wa msichana kwa sababu zisizo za kitabibu. Wakati mwingine huitwa kutahiriwa kwa mwanamke.

Ukeketaji hufanyika kama sehemu ya mila ya muda mrefu na imani za kitamaduni. Jamii nyingi ulimwenguni kote ziko zinaifanya iwe kinyume cha sheria.

## Namna gani ukeketaji huathiri afya?

Aina zote za ukeketaji huathiri au kuondoa utando wenye afya na zinaweza kusababisha madhara makubwa kwa muda au milele. Hii inaweza kujumuisha:

> maumivu, kutokwa damu, maambukizi

> ugumu wa kutoa mkojo

> matatizo katika hedhi

> maumivu wakati wa kujamiiana na hedhi

> shida ya kupata watoto

> matatizo wakati wa kujifungua

> maumivu ya kihisia na kisaikolojia.

**Wazazi wa wasichana wanaweza kuhisi shinikizo la familia au jamii kufanya ukeketaji hata baada ya kuja Australia. Ikiwa hii itatokea, kumbuka sheria ya Australia daima huchukua mkondo wake. Ukeketaji ni uharifu na adhabu kali zinatumika.**

Ukeketaji kwa Wanawake hauna faida za afya kwa wasichana au wanawake.

## Kupata msaada

Pata msaada mara moja ikiwa mtu yeyote unayemjua yuko hatarini kukeketwa au kupelekwa nchi nyingine ili kukeketwa. Unaweza:

> kuwasiliana na huduma. Wao ni wasiri. Unaweza kuomba mkalimani wa kike

> kupiga simu Polisi. Unaweza kuzungumza na polisi wa kike

> kupiga simu Kitengo cha Taarifa kuhusu Watoto Wanaonyanyaswa.

Ikiwa umekatwa au haujui kama umekatwa, unaweza kuzungumza na daktari wako, huduma ya afya ya wanawake au mfanyakazi wa afya kuhusu:

> masuala yoyote ya kimwili, ya kihisia au mengine

> njia za matibabu

> kuwa mjamzito au kutarajia kuwa mjamzito

> kuchunguza afya.

Tafuta msaada mara moja iwapo kuna msichana yupo katika hatari ya kukeketwa. Kuna huduma zinazoweza kusaidia.

## Huduma

### Ikiwa una wasiwasi juu ya usalama wa mtu

**SA Polisi (SA Police)**
000 ikiwa mtu yuko hatarini sasa
13 14 44 ikiwa kuna hatari, lakini siyo sasa hivi

**Simu kwa ajili ya kutoa Taarifa kuhusu Unyanyasaji wa Watoto (Child Abuse Report Line)**
13 14 78 muda wowote mchana au usiku
Kama wewe au yeyote anajua msichana aliye hatarini
www.childprotection.sa.gov.au/reporting-child-abuse

**Simu kuhusu Vurugu za Majumbani (Domestic Violence Crisis Line)**
1800 800 098 muda wowote mchana au usiku
Msaada vurugu, malazi ya dharura na uhamisho
http://womenssafetyservices.com.au

**Tume ya Kutoa Huduma za Kisheria SA (Legal Services Commission of SA)**
Simu kwa ushauri 1300 366 424, saa 3 asubuhi-saa 10.30 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa
Ushauri wa bure wa kisheria www.lsc.sa.gov.au

**Huduma ya Ukalimani na Tafsiri (Translating and Interpreting Service (TIS National))**
13 14 50 kwa wakalimani wa bure wa kwenye simu muda wowote mchana au usiku www.tisnational.gov.au

### Ikiwa unahitaji huduma za afya, msaada, taarifa au ushauri

**Huduma ya Afya ya Wakimbizi (Refugee Health Service)**
8237 3900 au 1800 635 566 (wanaoita kutoka vijijini) saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa
21 Market Street, Adelaide
Huduma ya afya kwa wakimbizi wapya na wanaotafuta hifadhi

**SHINE SA**
Sexual Healthline 1300 883 793 or 1800 188 171 (wanaoita kutoka vijijini) saa 3 asubuhi-saa 6.30 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa kwa ushauri wa siri
Habari katika lugha kadhaa www.shinesa.org.au

**Huduma ya Afya kwa Wanawake (Women's Health Service)**
8444 0700, saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa
47 Dale Street, Port Adelaide (pia Elizabeth and Hillcrest)
Kliniki za afya za siri za wanawake kwa bure www.whs.sa.gov.au

**Idara ya Mambo ya Nje na Biashara (Department of Foreign Affairs and Trade)**
1300 555 135 muda wowote mchana au usiku ikiwa wewe uko Australia na unahitaji msaada
+61 2 6261 3305, SMS +61 421 269 080 kama uko nje ya nchi
http://dfat.gov.au

**Kituo cha Tamaduni Mbalimbali kwa ajili ya Afya ya Wanawake Kutoka (Multicultural Centre for Women's Health)**
Zana ya Elimu ya Taifa kwa ajili ya Uelewa wa Ukeketaji ka Ukataji wa Sehemu za Siri za Kike (NETFA) www.netfa.com.au

Mwongozo huu rahisi wa Mzazi ni mmoja kati ya 9 iliyoundwa na Parenting SA kwa ajili ya familia kutoka kwenye jumuiya mpya zenye tamaduni mbalimbali na zinazoendelea kujitokeza Australia ya Kusini. Tungependa kushukuru mashirika mengi pamoja na familia ambazo zimechangia bure maarifa na utaalam kwenye Miongozo, hasa familia na wafanyakazi ambao picha zao zinaonekana ndani yake.
Parenting SA inashirikiana na Idara ya Elimu na Mtandao wa Afya wa Wanawake na Watoto.
**Simu (08) 8303 1660**
**www.parenting.sa.gov.au**
**Mwongozo Rahisi wa Wazazi unatolewa bure Australia ya Kusini**
**Muhimu:** Taarifa hii haikusudii kuchukua nafasi ya ushauri kutoka kwa mtaalamu.
© Serikali ya Australia ya Kusini Toleo la kwanza 01/2019.

Government of South Australia